# EDU SERIES EXAM

# KISWAHILI

**KISWAHILI STD 7**

# KISWAHILI DARASA LA SABA (7)

Muda**: Saa 1 Dakika 40**

Migomo ya wanafunzi __1__ shule __2___upili nchini __3__jambo ambalo linaathiri shule nyngi. Migomo __4___ aghalabu hufanyika muhula __5__ pili kabla ya mitihani ya __6__ muhula wa tatu. Wanafunzi wengi wanapohojiwa __7___ migomo, hutoa sababu ambazo hazina msingi kamwe. Ni wazi kuwa wanafunzi __8___ hugoma bila sababu maalum yenye uzito.wengi huwalaumu viranja na walimu wakali. Lakini ukweli ni kwamba ___9___ hukosa uzalendo kabisa _____mwao.

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | A. | kwa | B. | kwenye | C. | katika | D. | penye |
| 2. | A. | na | B. | mwa | C. | ya | D. | za |
| 3. | A. | imekuwa | B. | zimekuwa | C. | limekuwa | D. | litakuwa |
| 4. | A. | ile | B. | hii | C. | zile | D. | lile |
| 5. | A. | ya | B. | wa | C. | za | D. | la |
| 6. | A. | kitaifa | B. | kimataifa | C. | taifa | D. | mataifa |
| 7. | A. | kwa | B. | kuhusu | C. | katika | D. | na |
| 8. | A. | wenye | B. | wenyewe | C. | kwenyewe | D. | mwenye |
| 9. | A. | wao | B. | kwao | C. | vyao | D. | nao |
| 10. | A. | baina | B. | miongoni | C. | ndani | D. | mle |

Vituko vya zumbukuku ____11__ walimu kooni. Daima hakupenda kufanya kazi ___12____ ila ____13 ___ tu na kupiga na wanafunzi kufu ____14____. Naam! Mwalimu mkuu ____ 15____habari zumbukuku aliona kilichomtoa kanga manyoya.

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 11. | A. | viliwafikia | B. | viliwafika | C. | viliwafikisha | D. | vilifika |
| 12. | A. | yoyote | B. | lolote | C. | vyovyote | D. | chochote |
| 13. | A. | kupumzisha | B. | kupumzishwa | C. | kujipumzikia | D. | kupumzikia |
| 14. | A. | maji | B. | vijembe | C. | debe | D. | porojo |
| 15. | A. | alipofikiwa | B. | alipopashwa | C. | alipoletwa | D. | Alipofika |

**<u>Kuanzia nambari 16 hadi 30, chagua jibu lililo sahihi kulingana na maagizo</u>**

16. Chaguakiunganishi kifaacho kujaza pengo katika sentensi uliyopewa

    Aliupita mtihani huo____ hakusoma kwa bidii
    A. Licha ya
    B. Ingawaje
    C. Pasi na
    D. Almradi

17. Sehemu iliyopigiwa mstari katika neno ulilopewa ni

    A**<u>li</u>**mpiga
    A. Kiambishi cha wakati
    B. Kimbishi cha nafsi
    C. Liambishi cha ngeli
    D. Shina la kitenzi

18. Ngeli ya i-i ina jumuisha nomino zifuatazo isipokuwa


    A. Sukari B. mvua
    C. mihadarati D. chupa

19. Andika kinyume cha sentensi ifuatayo :-Juma alijenga nakuezeka nyumba yake vizuri

    A. Juma alijenga na kuezeka nyumba yake vizuri
    B. Juma alijenga wala kuezeka nyumba yake vizuri
    C. Juma alibomoa na kuezua nyumba yake vibaya
    D. Juma hakujenga na kuezeka nyumba yake vibaya.

20. Ni vazi lipi huvaliwa na wanawake pekee

    A. kocho B. kanchiri
    C. bwelasuti D. bombo

21. Ni sentensi ipi inayoonyesha “kwa” ya kitumizi .
    A. Maulidi anakaa kwa ndugu yake
    B. Maulidi aliadhibiwa kwa ujanja wake
    C. Maulidi aliinyywa chai wa kikombe
    D. Maulidi aliandamana moja kwa moja na mwalimu
22. Tambua alama ya uakifishaji katika neno ulilopewa
    Ng’ara
    A. Ritifaa　　B. parandesi
    C. nukta pacha　　D. koma
23. Chagua sentensi iliyo na matumizi mwafaka ya kirejeshi ‘’O’’ tamati
    A. Mwanafunzi ambaye asomaye kwa bidii hufaulu
    B. Mwanafunzi anayesoma kwa bidi hufaulu
    C. Mwanafunzi ambaye anasoma kwa bidi hufaulu
    D. Wanafunzi asomaye kwa bidi hufaulu
24. Mwalimu wetu wa somo la jamii alitupeleka mjini Nairobi kuzuru____ ili kuona vitu vya kihistoria na namna vina vyohifadhiwa.
    A. Gane
    B. Makavazi
    C. Dahalia
    D. Gulio
25. Eleza maana ya sentensi hii
    Nisingepika chakula ningeshinda njaa
    A. Alipika chakula akashinda njaa
    B. Hakupika chakula wala kushinda njaa
    C. Alipika chakula na hakushinda njaa
    D. Hakupika chakula akashinda njaa
26. Ipi si konsonati wala sauti kiswahi kati ya hizi
    A. /ch/　　B. /ny/
    C. /Q/　　D. /ng’/
27. 
    Umbo hili ni
    A. Pia B. Kishada C. Tao D. Kopa
28. Chagua methali iliyo na maana sawa na maelezo haya :
    Ni vizuri mtu kutosheka na kitu chake japo duni kuliko kutamami cha mwengine kilicho bora
    A. Bura yangu sibadili na
    B. Nazi bovu harabu ya nzima
    C. Kipya kinyemi ingawa kidonda
    D. Jungu kuu halikosi ukoko
29. Juma na Omari walipigiana simu kitenzi kilichopigwa mstari kipo katika kauli gani?
    A. kutendedsheana
    B. kutendea
    C. kutendana
    D. kutendeana
30. “ki” ya masharti imedhihirika kupitia sentensi ipi kati ya hizi
    A. Kitoto kichafu kiliogeshwa hadharani
    B. Mtoto mchafu alilia kitoto alipoogeshwa hadharani
    C. Mtoto mchafu akioogeshwa hadharani hulia
    D. Kikombe kilichonunuliwa kumepasuka

***soma kifungu kifutayo kisha ujibu maswali 31-40***

kila mapambazuko,alionekana barabarani mbioni. Alikuwa akifanya mazoezi yake kujiandaa kwa mbio za nyika. Jambo hilo alilifanya kwa ari na bidii zilizopita zile za mchwa. Alionyesha nia na azma ya kipekee.

Kwa miaka mitano mtawalia,alichekwa na kubezwa na wengi pale kijijini. Waliangua vicheko walipomuona akihema na kutweta huku jasho likimtiririka. Haya yalimwumiza sana moyoni lakini akajinyamazia tu. Aliwapa jicho tu.

Wengine walionekana kumuhurumia kuwa huenda hakua na akili timamu. Wengine walisikika wakisema kuwa masikini kaza alikuwa akiadhibiwa na mungu. Ilisemekana kuwa, akiwa mkembe wa umri wa karibu miaka kumi alitumwa akimbie dukani na mwendazake bibiye lakini akakataa. Eti akalaaniwa awe akikimbia kila asubuhi ikiwa adhabu.

Hakuna aliyekuwa na uhakika na jambo lile. Watu wengi walijiuliza mbona akaanza tabia hizo miaka mitano baada ya nyanya yake kwenda jongomeo!.

Baada ya mazoezi ya kabambe, kaza alianza kushiriki katika mashindano mbalimbali. Aliposhiriki mara ya kwanza, hakufua dafu. Ajabu kubwa alishika mkia licha ya bidii zake zote. Kumbe si lazima bidii ifuatwe na pato papo hapo!.

Alizidi kufanya mazoezi yake bila kufa moyo. Kadri alivyozidi mazoezi yake,ndivyo wengi walivyozidi kumcheka. Hakubwaga silaha. Alielewa kuwa,penye nia pana njia. Matendo yake yaliwashangaza wengi. Yote hayo waliyaona sawa na kuchota maji kwa pakacha.

Mwaka uliofuata,akiwa na umri wa miaka kumi na minane,alishiriki tena katika mbio za nyika. Alipata nguvu mpya alipong'amua kuwa ingawa hakuibuka mshindi,hali yake ilizidi kuimarika. Alizidi kupata ujuzi. Hilo liliwasha moto wa ufanisi moyoni mwake. Aling'amua kuwa papo kwa papo kamba hukata jiwe.

Si ajabu basi,nusu mwaka baadaye, kaza aliorodheshwa katika kikosi cha taifa cha kushiriki katika michezo ya olimpiki. Huo ukawa ndiyo mwanzo hasa wa kung'ara kwa nyota yake ya ufanisi. Nyota ambayo kwa miaka mingi ilikuwa haijang'ara kiasi cha kuonekana na wengi.

Dunia nzima alishuhudia kaza akinyakua nishani ya dhahabu katika michezo hiyo ya olimpiki. Kazi, kijana aliyelelewa kitovu cha ufukara, aliyebezwa na kutemewa mate,akajulikana kote duniani. Alivuliwa kofia hata na viongozi wa mataifa. Akawa mtu wa kutajwa. Akawa mtu wa kula katika hoteli za kifahari.

Miaka miwili baadaye, kaza akawa akinuka pesa. Maisha yake nay a aila yake yalibadilika. Akawasaidia wengi, wa mbali na karibu. Waliomucheka awali wakakosa uso. Wakaelewa kuwa, dhamira ni dira na nia zikiwa pamoja,kilicho mbali huja karibu.

**<u>Maswali</u>**

31. Kwa nini wanakijiji wengine walikuwa wakimcheka kaza?
    A. Hawakuelewa umuhimu wa mazoezi yake
    B. Walimuonea huruma alipokuwa akifanya mazoezi
    C. Walidhani alikuwa amelaaniwa
    D. Alikuwa masikini sana.
32. Baadhi ya wanakijiji walisikika wakisema kuwa kaza alikuwa akiadhibiwa kwa sababu gani?
    A. Hakuwa na akili timamu
    B. Akiwa mkembe alitumwa akimbie dukani na mwendazake bibiye lakini akakataa.
    C. Hakuwa mcha Mungu
    D. Aliumizwa moyoni na kuonyesha unyamavu
33. Kaza alianza kushirika mashindano ya nyika akiwa na umri upi?
    A. Miaka kumi na saba
    B. Miaka kumi na mitatu
    C. Miaka kumi na minne
    D. Miaka kumi na minane
34. Ni methali ipi mwafaka kuelezea tabia za kaza baada ya kushindwa katika jaribio la kwanza
    A. Kuvunjika kwa mwiko sio mwisho wa upishi
    B. Yakimwagika hayazoleki
    C. Asiyekujua hakuthamini
    D. Mbio za sakafuni huishia ukingoni
35. Kwa nini kaza alihisi uchungu moyoni
    A. alishindwa
    B. alichekwa
    C. alionewa
    D. alilaaniwa
36. kushinda kwa kaza kulitokana?
    A. Ujuzi,bidii na tajriba
    B. Umri mchanga
    C. Kutweta na kutiririka jasho
    D. Laana,kutweta na bidii
37. Yote hayo waliyaona sawa na kuchota maji kwa pakacha.ina maana kuwa?
    A. Walimuona kaza akilifanya jambo la busara
    B. Walimuona kaza kuwa mwenye bidii
    C. Walimuona kaza akijaribu kulifanya jambo lisilowezekana
    D. Walimuona kaza kuwa mtu aliyeyapenda mambo makuu
38. Ni nini maana ya neno KUTWETA
    A. Kupumua kwa nguvu
    B. kuchoka
    C. kutiririka jasho
    D. kupiga unyende
39. akawa mtu wa kula katika hoteli za fahari. inamaanisha
    A. kaza akawa mpenda kula sana
    B. kaza akawa mpenda anasa

C. kaza akawa mtu wa maringo
D. hadhi yake ya maisha ilipanda sana

40. ni methali ipi isiyoweza kutumika kueleza tabia za kaza.
A. Kuinamako ndiko kuinukako
B. Msafiri ni aliye bandarini
C. Mbio za sakafuni huishia ukingoni
D. Penye nia ipo njia

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50***

Uliwadia wakati wa wabunge,magavana,maseneta na wengineo kulingana na katiba mpya kurudi mashinani kwa waliowachagua wakiwa na ulimi wa sukari.hii ilikuwa ni kwa kutafuta kura na kujipendekeza kwa raia wote ili wachaguliwe kushiriki nyadhifa mbalimbali.

Ungewasikia wakiwarai raia kwa kuwaahidi kwamba wakimchagua mgombezi Fulani basi wote wataishi kwenye majumba ya ghorofa,nyumba zile zitakuwa na nguvu za umeme.wana wao watalipiwa karo hadi vyuo vikuu. Barabara zote zitakarabatiwa na kutiwa lami.

Ulifika wakati ambapo wapiga kura walipata kujua ukweli. Wakaelewa uongo wa baadhi ya wanasiasa-kwani penye uongo ukweli hujitenga. Wakatambua kuwa kuna wale ambao huwajibika wanaowawakilisha bungeni na wengine ambao huwazika wapiga kura katika kaburi la sahau pindi tu wanapotangazwa washindi.wale ndio maneno yao yamejaa matatizo mengi kama barabara mbovu, ukosefu wa maji, ufukara,ukosefu wa amani na ukosefu wa miundomsingi.yaani wana madhila chungu nzima.

Kwa wale wasiosinsia kazini,juhudi zao hutambulika kwani maeneo yao yamepiga hatua kimaendeleo.utawasikia waja wakisifia vitendo vyao. Wao huwafaa watu wa kwao kwa la jua na la mvua na hawawatelekezi mara kwa mara. Hufika mashinani kusikiliza shida za wananchi nao hufanya juu chini kuzitatua.wameelewa,kamba ya mbali haifungi kuni. Basi tuwajibike tubaini kazi ya mbivu na mbichi. Wanaofaa kutemwa nje watemwa wasalie watakaoliendesha dau letu hadi upeo wa juu zaidi.

41. Kulingana na aya ya kwanza wabunge hurudi mashinani
A. Kwenda kujulia watu hali
B. Kuwarai wapiga kura kuwapigia kura
C. Kutazama maendeleo waliyofanya
D. Kuomba usaidizi

42. ‘Kutia chumvi’ ina maana ya
A. Kueleza maneno magumu
B. Uongeza ukweli
C. Kusema maneno mengi yasiyo ya ukweli
D. Kunena maneno machache

43. Kulingana na kifungu, wanaosifiwa kwa vitendo vyao ni:
A. Wenye ulimi wa sukari
B. Wanaopotea baada ya uchaguzi
C. Wanaotia maneno ya chumvi
D. Wanaoendeleza sehemu walizochaguliwa

44. chagua jibu lisilo sahihi kwa mujibu wa kifungu
A. magavana huwakilisha gatuzi
B. wanaotafuta kuchaguliwa husema ukweli
C. wanasiasa wote huwafaa watu wa kwao
D. kila mpiga kura hutendewa aliyohaidiwa

45. Chagua kisawe cha neno amali jinsi lilivyo tumika katika kifungu
A. urembo B. kazi
C. kura D. wanasiasa

46. chagua methali iliyo na maana sawa na “kamba ya mbali haifungi kuni”
A. tenda wema nenda zako
B. ujanja wa nyani huishia jangwani
C. fimbo ya mbali haiui nyoka
D. haraka haraka haina baraka

47. chagua sifa ya mwanasiasa hodari
A. laghai
B. mwenye mabezo
C. mwajibikaji
D. mwenye maneno matamu

48. wabunge wanapoomba kura wanaahidi haya yote ila
A. kuleta nguvu za umeme
B. kutoa nafasi za kazi
C. kujenga ghorofa
D. kuchimbua barabara nzuri

49. kulingana na kifungu hiki wapiga kura wanajua
A. wanasiasa wanaowasahaulia mbali
B. baadhi ya wabunge
C. matokeo ya uchaguzi
D. kuongeza ukweli

50. kichwa mwafaka cha makala haya ni
A. nafasi za kazi
B. wanasiasa shupavu
C. uwongo wa wanasiasa
D. wakati umewadia